

NG'AMBO YA PAZIA LA WAKATI

 Ninataka kutangaza hapa ya kwamba maombi yenu yalijibiwa, mikutano kama tuliyoukuwa nayo wakati nilipoanza huduma, miaka mingi iliyopita. Kamwe sijawahi... Hata tusingeweza kuwaketisha watu. Na kupata viwanja vya maonyesho na kila kitu kingine, kungekuwako na wa kutosha mle kwenye saa tisa, kupajaza mahali hapo. Ingewalazimu kuyafunga malango, wasingewaruhusu kuingia. Tusingekuwa huko hadi saa moja. Mnaona? Maelfu tu wakimiminika kutoka kila mahali. Ninii tu... .

² Nami nilichukua siku tano za kwanza usiku kwenye mkutano wa mwisho, na kujenga tu kwenye Neno, nikaanza kutambua jinsi Neno lilivyokuwa na nguvu. Mnaona? Kwa sababu, Neno ni Mungu. Mnaona? “Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu.”

³ Sasa, Waebrania 4 ilisema hivyo, ya kwamba, “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili.” Mnaona? “Neno la Mungu ni kali kuliko, hata linachoma hata kuugawanya mfupa, na kukata, na kuyatambua mawazo ya nia, ya moyo.” Mnaona? Hivyo ndivyo, Neno la Mungu.

⁴ Ndipo kama kuna karama ambapo tunaweza tu kujituliza wenyewe; nalo Neno, Lenyewe, ambalo ni Kristo, Ambaye ni Neno, linaingia ndani yetu, na kuyatambua mawazo ya nia, kama vile mmeliona. Mnaona? Ajabu vipi. Halafu, kuona yale Yeye aliyofanya na jinsi alivyotubariki! Halafu basi ninii... .

⁵ Hilo, naona kwamba, kulijenga kwenye hilo Neno siku nne usiku, kuwaacha tu watu waketi kimya, halafu wapumzike tu, naye Roho Mtakatifu angewaita watu na kufanya mambo huko kwenye kusanyiko.

⁶ Halafu basi, kwenye usiku wa mwisho, Jumapili iliyopita alasiri, niliona mmoja wa misururu mikubwa sana ya uponyaji niliyopata kuona Marekani. Mnaona? Walikuwa... Nilimtuma Billy kule chini na kadi mia moja, na Gene na mia moja, na Leo na mia moja, na Roy na mia moja, kuzisambaza tu hizo kadi zote, yapata mia tano. Ndipo basi walipokuwa wameona Neno limeimarika, na yale lingefanya, halafu kudumu moja kwa moja kwenye Neno hilo sasa, nikawaleta jukwaani. Nami niliona wanaume na wanawake wakiitupa mikongojo yao, na kadhalika, na kuponywa kabla hata hawajafika jukwaani, kuona tu. Mnaona? Neno la Mungu lilikuwa tayari limetolewa, likapitia mle, na kujipenyeza Lenyewe katika Jumbe hizo tano, ama Jumbe nne, ndani ya mioyo yao, mpaka wakaliadini kwa moyo wao wote. Halafu, jambo pekee walilopaswa kufanya,

ni kuwa na namna fulani ya mawasiliano madogo, mnaona, kitu fulani, ndipo likawa halisi. Ndipo mara walipofika tu kwenye jukwaa hilo, wangeponywa papo hapo jukwa-... kabla tu hawajavuka jukwaa.

⁷ Ninaamini, ndugu hapa, nyote mnamfahamu Ndugu Ed, Ndugu Ed Hooper. Sivyoy? Ninyi kutoka Arkansas, huko chini? Alikutana... Yeye alikuwa pamoja nami katika sehemu za mwanzoni mwa huduma. Akasema, "Hii ilionekana kama nyakati za kale," akasema, "jinsi walivyokuwa wakifanya, miaka kadhaa ilivyopita."

⁸ Basi kulikuwako na watu waliokuwa na vivimbe ambavyo vilikuwa—vilikuwa namna *hiyo*, wakarudi, wazima. Vipofu, viziwi, bubu, kila namna ya mambo ambayo Bwana wetu aliyafanya. Hata haibidi kuwagusa hao watu. Neno linalotolewa linawagusa.

⁹ Ndipo Bwana akanipa Ujumbe ambao ningetaka kuuzungumzia kanisani, wakati mmoja, nitakaporudi, nikipata nafasi. Nina shughuli nyingi sana. Sasa inanibidi kuondoka tena, kesho, nikimngojea msichana huyu kuja. Na hata kabla sijalichukua sanduku langu la nguo nyumbani, kulikuwako na mtu fulani kule. Wala sijaketi chini tangu wakati huo, karibu sijaketi. Mnaona? Hata sijazungumza na familia yangu tangu niliporudi. Mnaona? Na ni—ni uchovu kweli. Nami ninawasihi nyote kuniombea, pia, kwamba Bwana atanisaidia kushikilia.

¹⁰ Sasa... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Kuona ndugu yetu hapa, mgonjwa sana, sana, amelazwa kwenye kitanda hiki cha wagonjwa. Nasi...

¹¹ Mtu fulani anatumia, katika muda mfupi, kutuchukua, kwenda Louisville. Ninawataka mkumbuke lile ombi, pia, msichana mzuri, ambaye, hajapata umri wa miaka kumi na minane. Yeye ni pacha, na msichana Mkristo shuleni. Nao hao wasichana wengine wangezungumza habari zake, mwajua, hao wasichana wawili, na kuwaambia jinsi walivyokuwa, sehemu ya maisha waliyokuwa wakiikosa, na jinsi wanavyopaswa kuishi kama hao wasichana wengine. Basi msichana mmoja aliweza tu kuyastahimili. Huyu mwingine alikuwa na kinyongo, naye akajisikia vibaya sana kulihusu, ndipo akaendelea kuzorota, na kuharibikiwa zaidi, naye anahofia hayo. Ndipo hatimaye akarukwa na akili. Nao... Yuko kwenye wadi ya wendawazimu. Mama na baba yake wanakuja, kidogo tu, kutoka Crandall, Indiana, kwenda kwenye hospitali hii ambako wanaenda kujaribu kumtuma, huko Madison, kesho.

¹² Sasa, m—msichana huyo, hakuna kasoro yoyote ya kimwili katika huyo msichana. Yeye... Hakuna kitu, kimwili. Ni mwenye afya kikamilifu. Lakini ni vigumu sana kulielezea. Na kwa kweli halielezeki. Jambo ni kwamba, roho yake

imetangatanga. Mnaona? Sasa, hu—huna budi kuishika roho yake na kuirudisha mahali pake. Mnaona? Kuna . . .

¹³ Kama vile, ndio kwanza tumalize kuzungumza hapa, majuma machache yaliyopita, jinsi ambavyo mfumo wa binadamu hufanya kazi. Jinsi ambavyo kuna hisi tano ambazo unaingilia humo mwilini, halafu tungeita milango mitano. Milango mitano, kama—kama vile dhamiri, dhana, na kadhalika, tunazolingilia nafsiini. Ndipo unapoingia kwenye roho, kuna mlango mmoja tu, na huo ni kupitia kwa hiari, ambalo linaliweka msingi huko nyuma kama vile mwanadamu alivyoubwa.

¹⁴ Unaweza kulipokea, ama unaweza tu kuliachilia liende. Unaweza kumkubali Kristo kama Mwokozi, ama umwache tu aende. Nawe ungali karibu na Mti ule, ule wa Uzima na ule wa mauti. Kila mwanadamu amewekwa mbele ya Mti huo, la sivyo Mungu angekuwa si mwenye haki kuweka mmoja pale, halafu asimpe huyo mwingine nafasi sawa ku—kuchagua mema na mabaya. Basi kila mmoja wetu ana nafasi hiyo.

¹⁵ Pia, katika hilo, roho, tunaweza kuponywa, ama hatuwezi kuponywa. Sasa, sio kwa sababu hakuna . . . kwamba hatujaponywa kulingana na Mungu. Tumeponywa. Kwa kuwa lile agano halina masharti. Naye tayari ameununua uponyaji wetu. Kwa hiyo, uponyaji wetu ni—ni kwa ajili yetu. Nai wetu. Sasa, ni kama tutachukua njia *hii*, kuliadini; ama njia *hii*, kutokuliadini kabisa. Sasa, kunayo njia hiyo moja tu tunayoweza kwenda Mbele za Mungu.

¹⁶ Sasa, mtoto huyu, mrembo, kipenzi cha mamaye. Mimi, ninii yangu . . . Loo, alikuwa ni mmoja wa marafiki zangu wasichana. Alikuwa maskini msichana mzuri, aliyetoka kwenye nyumba ya Kinazarayo yenye nidhamu kali, msichana mdogo mzuri sana. Naye ana mume mzuri. Ninamjua, pia, vizuri sana, yule mvulana aliyemwoa. Naye kidogo tu . . . Wanawalea watoto hao wapate kumtumikia Bwana, na kuwaweka shuleni. Nao kweli walikuwa wamewekwa msingi katika Kristo, kutokufanya mambo mabaya. Bali mambo yakawa hivyo.

¹⁷ Kwenye kuvurugika tu, kama tu vile mimi . . . niliangalia tu dakika chache zilizopita, na kumkazia macho maskini mvulana mdogo, alikuwa na jambo lile lile, kabisa. Na kwenye ninii . . . Tulishuka kwenda kule usiku mmoja, kwa Ndugu Wright, na Orville alikuwa a—amerukwa kabisa na akili. Naye, mwajua, wakati yeye angejaribu kunifukuza nyumbani; kadiri mimi na Orville tulivyo marafiki wazuri, kama tu vile ningalikuwa baba yake. Nilifunga ndoa ya baba na mama yake, pamoja. Naye angeruka tu na kupiga makelele, “Toka hapa! Toka hapa! Toka hapa!” Mnaona?

¹⁸ Sasa, kile kilichotubidi kufanya pale ni kuingia kwenye mstari wa roho na kuishika roho ya mvulana huyo. Mnaona?

Huzuni nyingi zilikuwa zimeingia kwenye maskini moyo wake. Yeye ni mchanga, naye alikuwa ameona mengi. Basi akarejeshwa tu moja kwa moja mahali anapopaswa kuwa. Mwaona? Katika siku chache, alikuwa—alikuwa ni mzima.

¹⁹ Sasa, hilo ni jambo lile lile unalopaswa kufanya kwenye hili. Nimeliona, nami ninajua hiyo ni kweli. Lakini sasa, ninii tu. . . Ni—ninawaomba ninyi nyote kuomba sasa, kwamba—kwamba Mungu atanisaidia kumpata maskini msichana huyu. Huko nje mahali, ambako hajui mahali alipo, kisha kumrudisha mahali pake. Mlango huo huja kupitia kwa imani. Mnaona, hawezi kuwa na imani kwa ajili ya nafsi yake. Hajui mahali alipo, ama chochote kile. Mnaona? I—itahitaji imani yetu hapa.

²⁰ Na sasa, katika jambo hilo, nguvu za kufufuka kwa Kristo, ambapo Yeye hutupa nafasi. Hapo ndipo, wewe, kwa njia moja, Neno la Mungu humchoma mwenye dhambi. Nalo halina budi kwenda zaidi ya kuhubiriwa kwa Neno linapotolewa. Hiyo ndiyo sababu nilitaka kuzungumza kidogo asubuhi ya leo kabla ya kuwaombea wagonjwa. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²¹ Mnakumbuka lile ono, sio muda mrefu uliopita, Bwana alilonipa, mwajua, kuhusu kuuona Upande ule mwingine? Hivi mnakumbuka asubuhi ile nilipokuwa nikishuhudia kuhusu kuona Upande ule mwingine? Vema, hiyo ilikuwa ni kweli.

²² Basi *Sauti* ya Wafanyabiashara wa Full Gospel limechapisha makala hayo, na kuweka picha upande wa nyuma wa huu ukurasa hapa. Nalo lina maandishi madogo yaliyoingizwa hapa chini, sehemu ndogo hapa chini, inayozungumzia huduma hii. Ambalo, hili ni gazeti la kimataifa linalochapishwa katika lugha nyingi mbalimbali. Nao waliutenga ukurasa wa mbele, na wa kwanza, juu ya ono hilo. Mnaona?

²³ Nami ninalo hapa, na laiti ungalichukua moja, na ungeweza kulisoma. Kisha usimame. . . Sikujua ni wangapi wangekuwa huku chini, hao ndugu, asubuhi ya leo. Nawe, basi, usipopata moja, vema, nenda tu ofisini. Wanayo kule ofisini. Nao walituruhusu kuchukua lundo la hayo, kuhusu: “Endelea kukaza mwendo.” Mnaona? Na hayo ndiyo yote yaliyo moyoni mwangu. Yote ninayoweza kusikia, ni, “Endelea kukaza mwendo.” Ng’ambo tu ya m—mto kuna N—Nchi bora. Basi hebu tuzidi kukaza mwendo mpaka tutakapokutana na Nchi hiyo.

²⁴ Sasa, nafikiri wana kuwekwa wakfu hapa kwa mtoto wa Ndugu Stricker na Dada Stricker. Kwa hiyo. . .

²⁵ Huyu anawafanya wangapi sasa, Dada Stricker? [Dada Stricker anasema, “Sita.”—Mh.] Jamaa sita wadogo. Hiyo ni maskini familia ya kupendeza.

²⁶ Na kwa hiyo wao. . . walikuwa wamishenari wetu huko—huko Afrika, hivi majuzi, wakarudi. Na watoto wao wote ni maskini jamaa wazuri sana. Nami naweza kuona huyu naye

ndivyo alivyo, pia, wakati wakimleta huku asubuhi ya leo kwa ajili ya ibada ya kuwekwa wakfu.

²⁷ Teddy yuko wapi? Teddy, waweza kuja hapa kwenye piano, kwa dakika moja tu, mwanangu? Basi—basi hebu tuimbe wimbo wetu, wimbo mdogo, mwajua, ule wimbo mdogo, ninaamini, tunaoimba, *Waleteni Ndani*. Hiyo ni kweli? “Waleteni ndani kutoka kwenye maeneo ya dhambi.”

²⁸ Na hiyo ni, sababu ya sisi kuucheza huu, ni kwa sababu kwamba sisi, kwa yote tuwezayo, wazazi, ni kuwaleta kwa ajili ya kuwekwa wakfu. Tunawaweka wakfu kwa Bwana na kuwaleta ndani wangali watoto wachanga, wasije wakapotelea kwenye eneo lile la dhambi. *Waleteni Ndani*. Hebu tuninii tu... Unaujua, Teddy? Hebu tuimbe tu kifungu kimoja chake sasa.

Waleteni, waleteni,
Waleteni kutoka kwenye maeneo ya dhambi;
Weleteni...

Kama kuna mwingine, mbona, mlete tu moja kwa moja.

Waleteni watoto wadogo kwa Yesu.

Waleteni, waleteni,
Waleteni kutoka kwenye maeneo ya dhambi;
Waleteni, waleteni,
Waleteni wanaotangatanga kwa Yesu.

²⁹ Ndugu Stricker na Dada Stricker, ninatambua ya kwamba mnajua maana ya wimbo huo, “kuwaleta ndani,” shauku kuu iko moyoni mwenu, kujaribu kuwaleta waliopotea kwa Yesu. Maskini mtoto wako mchanga, kama angekufa kabla hajawekwa wakfu, ama chochote kile, ameokoka, kwa vyovyote vile, kwa sababu Damu ya Yesu Kristo ilifanya hiyo pale Kalvari. Lakini katika kumbukumbu ya safari Yake kuu ya duniani, hapo alipoweka mikono Yake juu ya watoto na kusema, “Waacheni waje Kwangu,” hiyo ndiyo sababu mmemleta huyu mtoto asubuhi ya leo. Na kuweka matumaini ndani yetu, kwamba tungeweza kuomba maombi ya imani, kwa ajili ya huyu mtoto mdogo, katika kuwekwa wakfu kwa maisha yake kwa Mungu.

³⁰ Jina lake ni nani? [Baba anasema, “Marilyn Madge Stricker.”—Mh.] Marilyn Madge, Marilyn Madge Stricker. Ana umri gani? [Mama anasema, “Miezi kumi na mitatu.”] Miezi kumi na mitatu. Alizaliwa Afrika, hiyo ni kweli? [“Naam.”] Vema, jalia, kama kuna kesho, jalia mtoto huyu awe mmishenari kule, kwenye maeneo alimozaliwa. Na m—mtoto mdogo anayependeza. Waweza kuja, Ndugu Neville?

³¹ Na, Marilyn. Loo, jamani! Sikuzote nawapenda jamaa hawa wadogo. Huyu si ni jamaa mdogo anayependeza? U hali gani? U hali gani? Na tuinamisha vichwa vyetu. Nataka wewe, uweke mikono yako juu yake.

³² Baba yetu wa Mbinguni, tunakuletea Wewe mtoto Marilyn Madge Stricker, mtoto huyu mdogo mzuri aliyezaliwa kwenye maeneo ya umishenari, wakati vita vilipokuwa ni vikali. Naomba ya kwamba utambariki mtoto huyu. Katika Biblia, walikuletea watoto wadogo kama huyu. Uliwawekea mikono na kuwabariki, kasema, “Acheni watoto wadogo waje Kwangu, wala msiwazuie; kwa maana walio kama hao Ufalme wa Mbinguni ni wao.”

³³ Mama na baba wanamweka mikononi mwetu, leo hii. Sisi, kwa imani, tunapanda vipandio, huko ng’ambo, tunamweka mikononi Mwako, kwa imani. Yabariki maisha yake. Mpe maisha marefu, Bwana. Jalia awe mtoto wa Mungu. Jalia akutumikie kwa maisha yake yote, kila mshipa wa utu wake, awe mtumishi wa Kristo. Lijalie, Baba. Mbariki baba na mama yake, ndugu na dada zake wadogo. Jalia wasimame, pia, na wawe familia nzuri sana kwa utumishi wa Mungu.

³⁴ Baba, tunamkabidhi mtoto Marilyn Madge Kwako, katika Jina la Yesu Kristo, kwa maisha ya utumishi. Mbariki, na baba yake, na mama yake, na wapendwa wake. Pia jalia waishi muda mrefu, maisha yenye furaha katika utumishi Wako. Katika Jina la Yesu. Amina.

³⁵ Mungu akubariki, Ndugu Stricker. Mungu akubariki. Baraka juu ya maskini msichana mdogo.

Asante, Teddy, jamani.

³⁶ Nawapenda watoto wadogo. Nanyi je?

³⁷ Ni wangapi kamwe hawakusikia lile ono alilonipa Bwana? Hebu tuone mkiinua mikono yenu, ambao kamwe hawakulisikia. Ndugu Neville, unacho kitabu chako kidogo hapo, labda, labda ungewasomea hilo papa hapa, kwa dakika moja tu ama mbili zijazo. Ninaamini ni. . . Papa hapa tu, ukiweza.

³⁸ [Ndugu Neville anasoma kutoka kwenye toleo la Februari, 1961 la *Sauti ya Wafanyabiashara wa Full Gospel*—Mh.]

³⁹ [Hivi majuzi asubuhi nilikuwa nimelala kitandani mwangu. Nilikuwa ndio kwanza niamke usingizini, nami nikaweka mikono yangu nyuma ya kichwa changu na kupumzisha kichwa changu kwenye foronya. Ndipo nikaanza kushangaa itakuwaje kwenye ng’ambo ya pili. Nikatambua kwamba nilikuwa nimeishi zaidi ya nusu ya maisha yangu kama nikiishi kuwa wa rika ya watu wangu, nami nilitaka kufanya mengi zaidi kwa ajili ya Bwana kabla sijaondoka kwenye maisha haya.]

⁴⁰ [Nikasikia Sauti ikisema: “Ndio kwanza unaanza tu! Piga vita! Endelea kutia bidii!” Nilipokuwa nimelala pale nikiyatafakari maneno hayo, niliwazia ya kwamba ndiyo kwanza nidhanie kwamba nilisikia Sauti. Tena hiyo Sauti ikasema: “Piga vita! Endelea kusonga mbele! Endelea kusonga mbele!” Ningali siamini, nilidhani inawezekana niliyasema hayo

maneno mwenyewe. Nikaweka midomo yangu katikati ya meno yangu na kuweka mkono wangu juu ya kinywa changu na kusikiliza. Ile Sauti ikasema tena: “Zidi tu kukaza mwendo! Laiti ungalijua tu yaliyo mwishoni mwa safari!” Nilionekana kusikia muziki na maneno ya wimbo wa kale, unaojulikana:]

[“Nina huzuni na tamaa ya kwenda nyumbani,
nami nataka kumwona Yesu,]

[Ningetaka kusikia hizo kengele za bandarini
zikilia.]

[Ingeiangazia njia yangu na kuondoa woga
wote.]

[Bwana, jalia niangalie ng'ambo ya pazia la
wakati!”]

⁴¹ [Ndipo hiyo Sauti ikauliza: “Ungetaka kuangalia ng'ambo tu ya pazia?” Nikajibu: “Lingenisaidia sana!”]

⁴² [Lililotukia siwezi kusema. Kwamba nilikuwa katika mwili ama nje, ama kwamba ilikuwa ni kuhamishwa, sijui mimi, bali halikuwa kama ono lolote nililopata kuona. Ningeweza kuona mahali nilipopelekwa na ningeweza kujiona nimelala pale nyuma kitandani mwangu. Nikasema: “Hili ni jambo la ajabu!”]

⁴³ [Kulikuwako na idadi kubwa ya watu nao walikuja mbio kunisalimia, wakipaza sauti: “Loo, ndugu yetu wa thamani!” Kwanza walikuja wasichana, walionekana wako kwenye umri wa miaka ishirini ya mwanzoni, nao wangenikumbatia na kusema: “Ndugu yetu wa thamani!” Vijana wanaume, katika upeo wa ujana, wenye macho yaliyometameta kama nyota kwenye usiku wenye giza, wenye meno meupe kama lulu, wakanikumbatia, wakisema, “Ndugu yetu wa thamani.”]

⁴⁴ [Kisha nikaona kwamba mimi, pia, nilikuwa nimekuwa kijana tena. Nikajiangalia pale na kugeuka na kuangalia nyuma kwenye mwili wangu mzee uliolala kitandani huku mikono yangu ikiwa nyuma ya kichwa changu. Nikasema: “Siyaelewi haya!”]

⁴⁵ [Nilipoanza kujaribu kutambua mahali nilipokuwa, nilianza kutambua ya kwamba hapakuwapo na jana wala kesho kule. Hakuna mtu aliyeonekana kuchoka. Wakati umati wa wasichana waremba sana niliopata kuona ukinikumbatia kwa mikono, niligundua kulikuwako tu na upendo mkuu ulionikumba wala si uvutio wa kimwili kama kwenye tabia za wanadamu. Niliona wasichana hawa wote walikuwa na nywele zilizofikia viunoni mwao nazo sketi zao zikafikia miguuni mwao.]

⁴⁶ [Baada ya haya, Hope, mke wangu wa kwanza, alinikumbatia, na kusema: “Ndugu yangu wa thamani!” Kisha msichana mwingine akanikumbatia naye Hope akageuka na kumkumbatia msichana huyo. Nikasema: “Sielewi haya. Hiki ni kitu tofauti kabisa na upendo wetu wa kibinadamu. Sitaki kurudi kwenye mwili huo wa kale kitandani.”]

47 [Ndipo Sauti ikasema nami: “Huu ndio ulihubiri kwamba ndivyo alivyo Roho Mtakatifu! Huu ni upendo mkamilifu. Hakuna kitu kinachoweza kuingia Humu pasipo huo!”]

48 [Kisha nikatwaliwa juu na kuketishwa mahali pa juu. Kote kunizunguka kulikuwako na idadi kubwa ya wanaume na wanawake katika upeo wa ujana wao. Walikuwa wakilia, kwa furaha: “Loo, ndugu yetu wa thamani, tuna furaha sana kukuona hapa!” Nikawazia: “Sioti mimi, kwa kuwa ninaweza kuwaona watu hawa na ninaweza kuuona mwili wangu umelala kule nyuma kitandani.”]

49 [Ile Sauti ikasema nami: “Unajua imeandikwa katika Biblia ya kwamba manabii walikusanywa pamoja na watu wao.” Nikasema: “Naam ninakumbuka hilo katika Maandiko, lakini hakuna wengi hivi wa Branham.” Ile Sauti ikajibu: “Hawa si wa Branham. Hawa ni waongofu wako, wale uliowaongoza kwa Bwana. Baadhi ya wanawake hawa unaowazia ni wachanga sana na warembo walikuwa na zaidi ya umri ya miaka tisini ulipowaongoza kwa Bwana. Si ajabu wanapaza sauti, ‘Ndugu yangu wa thamani!’” Ndipo huo umati ukapaza sauti pamoja: “Kama usingalijitokeza na Injili, tusingalikuwa hapa!”]

50 [Nikauliza: “Loo, yuko wapi Yesu? Ninataka kumwona!” Hao watu wakajibu: “Yeye yuko juu zaidi tu kidogo. Siku moja atakuja kwako. Wewe ulitumwa kama kiongozi, na wakati Mungu atakapokuja, Yeye atakuhukumu kulingana na mafundisho yako.” Nikauliza: “Hivi Paulo na Petro watalazimika kusimama kwenye hukumu hii pia?” Jibu lilikuwa: “Naam!” Nikasema, “Nimehubiri yale waliyohubiri. Sikuondoka Kwake kwenda upande mmoja ama huo mwingine. Ambapo walibatiza katika Jina la Yesu, nilifanya hivyo pia; ambapo walifundisha Ubatizo katika Roho Mtakatifu, nilifanya hivyo pia. Lolote walilofundisha, nilifundisha, pia.”]

51 [“Tunajua hilo,” hao watu wakalia, “nasi tunajua ya kwamba tunarudi duniani pamoja nawe siku moja. Yesu atakuja na kukuhukumu kulingana na Neno ulilotuhubiria. Ndipo wewe utatukabidhi Kwake, nasi sote pamoja tutarudi duniani kuishi milele.” Nikauliza: “Itanibidi kurudi duniani, sasa?” Wakajibu: “Naam, bali endelea kukaza mwendo!”]

52 [Nilipoanza kuondoka kwenye mahali hapo pazuri, pa furaha, kadiri macho yangu yalivyoweza kuona, watu walikuwa wakinijia wapate kunikumbatia, wakilia: “Ndugu yangu wa thamani!”]

53 [Mara nilikuwa nimerudi kitandani tena. Nikasema: “Loo, Mungu, nisaide! Kamwe usiniache nipatane kwa Neno. Jalia nidumu moja kwa moja katika Neno. Sijali yale mtu mwingine yeyote afanyayo, Bwana, jalia nikaze mwendo kwenda kwenye mahali hapo pazuri, penye furaha!”]

54 [Nimeshawishika zaidi ya hapo awali maishani mwangu ya kwamba itahitaji upendo mkamilifu kuingia mahali pale. Hapakuwapo na wivu, hakuna uchovu, hakuna maradhi, hakuna umri wa uzeeni, hakuna mauti. Ila tu upeo wa uzuri na furaha.]

55 [Lolote ufanyalo, weka kando kila kitu kingine mpaka upate upendo mkamilifu! Ufikie mahali ambapo unaweza kumpenda kila mtu, hata kila adui. Haidhuru kama ndege inayumbayumba, radi inamulika, ama bunduki za adui ziko juu yako, mambo haya hayajalishi: upate upendo mkamilifu!]

56 [Endapo hujaokoka, mkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wako sasa! Endapo hujabatizwa katika maji, batizwa sasa! Endapo hujapokea Ubatizo katika Roho Mtakatifu, upokee sasa! Kaza mwendo uufikie huo upendo mkamilifu ambao utakupeleka mahali hapo pazuri na pa furaha ng'ambo ya pazia la wakati!]

57 [Ndugu Neville amemaliza kusoma. Hapa chini, Ndugu Branham anarejea kwenye “maandishi madogo yaliyoingizwa” ambayo Ndugu Thomas R. Nickel, Mhariri wa Sauti ya Wanaume wa Full Gospel, aliweka kwenye ukurasa wa kwanza wa hayo makala, ambayo yanasema hivi: “Kuhusu picha kwenye jalada la mbele: Katika Siku za Biblia, kulikuwako na watu wa Mungu ambao walikuwa ni Manabii na Waonaji. Lakini katika Kumbukumbu zote Takatifu, hakuna mmoja wa hawa aliyekuwa na huduma kubwa kuliko ile ya William Branham, Nabii na Mwonaji wa Mungu, ambaye picha yake inaonekana kwenye jalada la mbele la toleo hili la Sauti ya Wanaume wa Full Gospel. Branham ametumiwa na Mungu, katika Jina la Yesu, kuwafufua wafu!”—Mh.]

58 (Asante, Ndugu, kwa ajili ya hilo.) Hiyo ni... Nilidhani, labda, baadhi yenu mngeweza kulisoma. Basi kama huna hicho kitabu kidogo, mbona, waweza kukipata.

59 Halafu kwenye...papo hapo chini ya ukurasa, yeye alitia maandishi madogo kuhusu hiyo huduma pale. Sijui kama mliyaona, ama la, papo hapo chini, ukiisha kusoma hayo. Chini kabisa, maandishi madogo yaliyoingizwa hapo chini. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

60 Sasa, hilo linaenda katika karibu kila lugha chini ya mbingu, mnaona, ku—kusomwa kote ulimwenguni.

61 Sasa, “Nini—nini...Vema,” mnasema, “kwa nini useme hivyo, Ndugu Branham, kabla hujawaombea wagonjwa?”

62 Ni kwa sababu ya jambo hili: ili tuweze kujua ya kwamba jitihada zetu si bure. Mnaona? Inatupasa kumkaribia Mungu kupitia kwenye mkondo huo wa upendo na imani. Imani hutupeleka kwenye mkondo huo. Upendo ndio unatuingiza ndani.

Samahani. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

⁶³ Sasa, mnafikiri ya kwamba Mungu angeninii...Sasa hebu...Sasa, imani yako inafikia mahali sasa, unafikiri ya kwamba...Ungewazia nini sasa kama jitihada zote ambazo ninii...maskani hii na makundi haya ya watu hapa yametoa, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu? Kuna wengi hapa ambao mmewanyima kitu watoto wenu, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Kuna wengi hapa ambao wameenda bila nguo, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Kuna wengi ambao wamepitia kwenye dhoruba, na kutembea bila viatu miguuni mwao, wapate kufika hapa maskanini, hiyo ni kweli, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

⁶⁴ Ungeweza kuwazia mwanasanaa akitia rangi picha kuu, nzuri, hata ikawa adhimu, kisha airarue tu? Huyu mwanasanaa angekuwa na kasoro. Ungeweza kuwazia mtunzi akiandika wimbo mpaka ukawa adhimu, kisha aurarue tu muziki wa—wake? Huyu mtunzi angekuwa na kasoro. Mnaona? Mungu hana kasoro. Mungu hafanyi kitu kama hiki, apate tu kukirarua na kukitupilia mbali. Ni kwa ajili ya Ufalme Wake. Ni kwa ajili ya Utukufu Wake.

⁶⁵ Kila mmoja wetu anatimiza sehemu yake katika picha hii na katika wimbo huu. Sisi ni sehemu za Ufalme wa Mungu. Na hiyo ni kusema, ya kwamba tunaweza kutimiza sehemu zetu, mradi tu tunatambua tulipo kimahali, mahali hapa ni petu, kisha tukae papo hapo katika mahali hapo. Na mahali pamoja tupajuapo, ni katika upendo, kwa maana huo ndio unaoifanya hiyo picha.

⁶⁶ Sasa, ni vigumu unapoyaona maono haya jinsi hii, na kadhalika, kufahamu yale—yale yaliyo kwenye Upande ule mwingine. Laiti ningalijua. Huyu mtu aliyeingiza maandishi haya hapo chini, kusema ya kwamba manabii wa kale, jinsi walivyoyaona maono haya, na kadhalika, na jinsi ambavyo, leo hii, kupita hata yale...Hatuwezi kulielewa, bali Bwana ameturuhusu kupenyeza humo na kuona hayo ni nini.

⁶⁷ Sasa, enyi marafiki, sikuwa nimelala. Nami, kati yangu tu na ninyi, na kanisa hili hapa, sikuwa katika ono. Ninajua ono ni nini. Mengine hapa, juma lililopita tu, mengine, yalikuwa kadiri ya mara thelathini, usiku mmoja, yangetokea. Unaweza kuwazia uzito ulio juu yako. Inakutia wasiwasi, hakika.

⁶⁸ Vipi kama ulihudhuria mkutano kama huo, na lile jukumu tu, kama mkutano uliendelea vizuri ama la, lilikuwa juu yako, ju—jukumu tu? Inakubidi kumjibu kila mhudumu, kila swali, kila kitu. Huo mkutano ukiendelea vizuri ama vibaya, ni jukumu lako tu, peke yako. Angalia kile hilo lingekufanyia.

⁶⁹ Na kuna baadhi ya wenzangu, wakiuza tu vitabu, na kadhalika, wanashikwa na wasiwasi sana, ingewabidi kwenda nyumbani, unaona, wapumzike, wasingekuwa kanisani usiku huo. Jamani! Loo, ni vibaya sana. Kama vile binti mkwe wangu, msichana mzuri Mkristo, Loyce. Kwa—kwa kwenda tu mkutanoni, kusudi tu...Kwa majuma manane, ama majuma

saba, sikuzote namna hiyo, ilimbidi kulala kitandani siku moja ama mbili, mnaona, bila jukumu. Mnaona? Billy, kusambaza tu kadi chache za maombi, na amevurugika kabisa.

⁷⁰ Lakini, mnaona, uzito wote uko juu yangu. Inanibidi kuwategemea ninyi mniombee. Mnaona? Mbali na hayo, wanadai ya kwamba—ya kwamba dakika ishirini za—za kuhubiri, chini ya upako, zinalinganishwa na saa nane za kazi ngumu, kwa mwili wako. Mimi nahubiri muda wa saa mbili hadi tatu usiku mmoja; wakati mwingine mara tatu kwa siku. Mnaona?

⁷¹ Halafu basi vipi kuhusu ono moja? Ono moja lilimfanya Bwana wetu Yesu kuwa dhaifu. Hiyo ni kweli. Biblia ilisema mwanamke aliligusa vazi Lake, likamfanya dhaifu. Vema, ikiwa ono moja litamfanya dhaifu, Yeye, Mwana wa Mungu; vipi kuhusu mimi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema, thelathini ya hayo yangefanya nini katika usiku mmoja? Mnaona? Ni...Kama tungalisimama tu na kuwazia, imepita mwanadamu yeyote. Mwili wa mwanadamu hauwezi kustahimili hayo. Ningekuwa kwenye hospitali ya wendawazimu mahali fulani, nikikigongesha kichwa changu kwenye kuta. Mnaona? Ni—ni udhaifu mkubwa ambao huwezi... Ni udhaifu wa ndani, mnaona, ambao unakuua tu.

⁷² Sasa, lakini ungesukuma nini basi? Huenda nikasema hivi. Ninamwona Ndugu na Dada Cox, pale, Rodney na mke wake, na dada, hapa, kutoka huko nyuma, waongofu wapya. Kunayo Nchi, huko ng'ambo tu mahali fulani, ambayo kama ungeweza kamwe kuwazia tu niani mwako na kupata mtazamo Wake, Ndilo jambo tukufu kuliko yote. Linastahili kila jitihada tunayoweza kuweka. Mnaona?

Sasa, kabla ya kuwaombea wagonjwa, huenda nikasema jambo hili.

⁷³ Vipi kama mtoto mchanga, kabla hajazaliwa...Hebu tumchukue huyo. Mtoto mchanga ambaye ameishi tumboni mwa mamaye, kwa miezi hii tisa, naye mtoto huyo angeweza kuwazia? Angesema, "Wajua nini? Wananiambia ninakaribia kuzaliwa. Vema, nitafanya nini huko nje? Sijui lolote ila mahali hapa ninamoishi hapa. Ninapata nguvu zangu kutoka ndani. Basi nitapataje riziki huko nje? Wananiambia kuna jua linalowaka. Wananiambia ya kwamba watu huko nje wanatembea huku na huku. Nami sijui chochote ila mahali hapa. Hapa ndipo pote nijuapo, mumu humu tu—tumboni mwa mama yangu. Hapa ndipo nilipolelewa. Hapa ndipo pote nijuapo, ni mumu humu ndani ya tumbo hili. Nao wananiambia ya kwamba kuna nafasi mara nafasi!" Vema, maskini mtoto huyo mchanga angehofia sana, kuzaliwa. Hiyo ni kweli? Angehofia sana, maana anakuja mahali hajui chochote kupahusu, ambapo ni adhimu, adhimu mara mamilioni, ukilinganisha na mahali amekuwa akiishi.

Asingejua yote hayo yanahusu nini. Angesema, “Vipi, nitafanya nini?” Angehofia kabisa, kuzaliwa.

⁷⁴ Lakini, sisi tunaishi huku nje, vema, sisi tuliokuwa huko nyuma wakati mmoja, tusingerudi huko kwa vyovyote vile. Tusingetaka kurudi kwenye tumbo la mama tena. Mnaona? La. Tusingetaka kufanya hivyo.

⁷⁵ Na hivyo ndivyo tu ilivyo tunapokufa, ewe rafiki. Ee Mungu! Mnaona? Unazaliwa katika Mahali fulani. Hujawahi kuwa Huko. Huwezi kupafahamu, jinsi palivyo pakuu. “I—itakuwaje Huko nje? Mimi. . .” Na jambo pekee linalonifanya kutambua, ama wewe kutambua, ni ule mguso mdogo wa Uzima, kama vile roho inavyoingia katika mtoto mchanga ndani ya tumbo la mama yake. Mnaona? Ndiyo njia pekee tunayoweza kuelewa ile Nchi kuu huko ng’ambo ni nini, wakati hakuna maradhi, hakuna huzuni, hakuna mauti, hakuna uzee, hakuna chochote. Loo, jamani! Mbona, mara ukiisha kufika Kule, kamwe usingetaka kurudi mahali kama hapa, si zaidi ya vile mtoto mchanga angetaka kurudi kwenye tumbo la mama yake. Mnaona? Ni kuu zaidi sana Upande ule mwingine, mnaona, Huko nje. Hutuwezi kulielewa, la hasha, hatuwezi. Mbona, jinsi mtoto huyo mchanga asingeweza kuwazia, vivyo hivyo na sisi hatuwezi kuelewa ni mambo gani yangekuwa Huko nje, mnaona, kwa sababu tuko kwenye tumbo la ardhini, tukiwa tayari kuzaliwa wakati mmoja, tuingie kwenye Ufalme mpya, katika Ulimwengu mpya.

⁷⁶ Na hivyo ndivyo ninavyojisikia kuhusu maono hayo na vitu kama hivyo, ama chochote kile kilichonipata siku hiyo nilipovuka kule, upande wa nje tu, na kuona vile Huko kulivyokuwa, kisha nikarudi nikaingia humu.

⁷⁷ Ungeweza kuwazia ukiwa mtoto mchanga na—na ulikuwa na u—ufahamu kile, jinsi kulivyokuwa adhimu huku kutembea huku na huku, kuona miti ikichanua, ndege wakiimba, jua likiwaka, na maisha kama haya, halafu ikubidi kuzuiliwa tumboni? Mbona, usingetaka kurudi, hata kidogo.

⁷⁸ Vema, basi, sisi, ma—mawazo yetu yangeingia ganzi, upande huo, ama kujaribu kuwazia hicho ni kitu gani Huko. Wakati, Maandiko yanasema, “Jicho halijaona, sikio halijasikia, wala halijaingia katika moyo wa mwanadamu yale Mungu amewawekea, akiba, wampendao.” Mnaona? Kwa hiyo tunajua ni adhimu Upande ule mwingine. Siku moja, mauti, yale tunayoita mauti, yatatupatia kule Kuzaliwa upya, nasi tutaingia kwenye Ulimwengu huo mwingine, Upande ule mwingine.

⁷⁹ Ndugu George, hutakuwa mzee, kiwete huku, Kule. Na Ndugu na Dada Spencer, na wengine kama baadhi yetu walio na umri mkubwa zaidi, na kadhalika, basi tutakuwa vijana, Kule, milele. Maskini huu. . .

Joho hili la mwili nitaliangusha, na kufufuka
 Na kunyakua tuzo la milele;
 Na kupiga makelele, wakati nikipitia hewani,
 Kwaheri, kwaheri, wakati mzuri wa maombi.

⁸⁰ Yote yamekwisha, basi. Hakuna tena usiku mrefu wa maombi, hakuna tena. Kuingia tu katika umri huo mdogo, wenye furaha kuwa Kule, sio tu kwa mwaka mmoja, au miaka hamsini, au miaka milioni moja, lakini tukiweko Kule miaka bilioni mia moja, hata hatutakuwa tumeanza hata kidogo. Hivyo tu. Basi kwa nini tusiwe na furaha asubuhi ya leo? Kwa nini tusishangilie? Kwa nini tusijinufaishe na kila kitu kikuu ambacho Mungu ametupatia?

⁸¹ Huu hapa uponyaji wa Kiungu. Kwa nini Yesu akapigwa; kuirarua hiyo picha, kusema, "Hakuna kitu kama hicho kwake"? Mwili wake ulipigwa kule, mifupa ikatokeza, kwamba, "Kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." Hebu tusiirarue hiyo picha, asubuhi ya leo. Hebu tuikumbatie, tuikubali.

⁸² Sasa, ndugu, na kila mmoja wenu sasa atakayeombewa, kama tu mtasimama kuyazunguka madhabahu. Wakati ujumbe ulipokuwa ukitolewa, dakika chache zilizopita, kupitia ufasiri na lugha, kwamba tungeweka mikono juu ya wagonjwa na kuziona kazi kuu za Mungu.

⁸³ Sasa, ndugu yetu, haikubidi kusimama, ndugu, hapo unayelala kwenye kitanda cha wagonjwa. Tutakuja kwako.

⁸⁴ Lakini kama kuna wengine wowote hapa wa kuombewa, wangetaka kusimama karibu na madhabahu, wakati mimi na ndugu tukiomba na kuweka mikono juu ya wagonjwa, njoo sasa hivi. Basi kumbuka, ikumbatie picha hiyo, "Kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa."

⁸⁵ "Silielewi, Bwana." Hakika, huelewi. Ungali kwenye tumbo la uzazi la duniani bado.

⁸⁶ Lakini Yeye alifanya hayo maandalizi. Wala asingechukua... Kwa nini akapigwa? Kuirarua tu hiyo picha, ama kuurarua huo wimbo, kuutupilia mbali? La, bwana. Yeye alipigwa, akajeruhiwa, akatokwa na damu, tupate kuponywa. Na kwa jambo hilo, sisi, "Mapigo Yake, tumeponywa," kila mmoja wetu. Sasa, wakati mkija, mkikusanyika madhabahuni kwa ajili ya maombi.

⁸⁷ Sasa, wingi wa huu uinjilisti wa ajabu sana wa Kimarekani, na kuzungumza juu ya, "Inakupasa kufanya *hili*, kufanya *lile*."

⁸⁸ Lipo jambo moja ninalotaka kuwa mwaminifu kwako kulihusu, rafiki yangu. Hilo jambo, jinsi Mungu anavyoponya, ni juu ya msingi wa kumtumikia Yeye. Mnaona? Ni juu ya msingi wa kumtumikia. Hatuna budi kuukubali uponyaji wetu juu ya msingi, wa, tutamtumikia tukiisha kuponywa. Sasa, Biblia ilisema, "Ungameni makosa yenu, ninyi kwa ninyi. Ombeaneni,

mpate kuponywa.” Mnaona? Ni juu ya msingi, utamtumikia Mungu. Wengi wenu hapa, labda, wako katika hali ya kufa, na wewe—wewe huna budi kufa kama jambo fulani halitukii. Ndipo ninawatakeni, moyoni mwenu. . .

⁸⁹ Sasa, huenda tukawapaka mafuta, huenda tukawaombea, mimi pamoja na mchungaji, tuombe maombi ya imani, tufanye yote tuwezayo, bali halitafaa kitu mpaka wewe mwenyewe uingie katika ushirika pamoja na Kristo. Unaona? Inakupasa kuingia kwenye ushirika huo, kwamba, “Mimi, Bwana. . .”

⁹⁰ Ninamwona m—m—msichana akitembea pale sasa hivi. Yeye alikuja hapa, si muda mrefu uliopita nyumbani, akiwa na kitu kama uvimbe, ama ugonjwa wa Hodgkin. Naye ni Mmethodisti, kwa imani. Ninaamini hiyo ni kweli, sivyo, dada? Naye alikuwa na uvimbe mkubwa ubavuni. Na sasa yule pale amesimama, amepona.

⁹¹ Ninamwona Dada Weaver amesimama hapa, alikuwa mmoja wa wenye ugonjwa mbaya sana wa kansa niliopata kuona, maishani mwangu mwote. Jambo la kwanza nililomwuliza, “angebatizwa katika Jina la Yesu Kristo,” na kuzitubu dhambi zake. Nilipomwingiza katika maji haya hapa, ilibidi nimshikilie; alikuwa amekonda sana, mikono yake, vitu vidogo tu. Basi akabatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Na hiyo imekuwa angalau miaka kumi iliyopita, sivyo, dada? [Dada Weaver anasema, “La. Hiyo imekuwa miaka kumi na sita iliyopita.”—Mh.] Miaka kumi na sita iliyopita. Miaka kumi na sita ya maisha ya nyongeza, kwa sababu alikuwa tayari kuja katika utii. Wakati madaktari walio bora sana wa karibu hapa. . .

⁹² Mbona, daktari wake mwenyewe aliniambia. Wakati, nilimwambia—nilimwambia, kasema, “Amepona.”

⁹³ Kasema, “Loo, loo! Atakufa kwa kansa, katika majuma machache. Usijali juu ya hilo. Atakuwa ameondoka. Majuma mengine machache, atakuwa ameondoka.” Naye tayari amempa tu yapata siku moja kuishi. Naye huyu hapa, leo hii, baada ya miaka kumi na sita, amesimama madhabahuni. Ningesema nini zaidi, zaidi na zaidi, na zaidi na zaidi!

⁹⁴ Sasa, Mungu hafanyi hivyo tu kwa mmoja wa watoto Wake, wala hafanyi hilo kwa watoto wengine. Hufanya hivyo kwa ajili ya watoto Wake wote. “Atakaye na aje.” Ni. . . Umealikwa Kwake. Sasa, “Maombi ya imani yatamwoko mgonjwa huyo.” Biblia ilisema hivyo.

⁹⁵ Sasa—sasa, kama. . . kile ninachotaka mfanye, ni kukiri makosa yenu kwa Mungu, na kusema, “Bwana, niponye mimi.” Kama hamjawahi kuongoka, itoeni mioyo yenu kwa Kristo. Na kama hujawahi kubatizwa, katika maji, katika Jina la Yesu Kristo, kidimbwi kiko tayari. Unaona?

⁹⁶ Naye msichana huyu upande wa pili wa huu mtaa hapa; wakati maskini yule kafiri alipoongoka kwake.

Wakati alipokuwa amelala...walimpeleka nyumbani kutoka Silvercrest, akiwa na TB, akifa. Ndipo niliposhuka kule, naye Bwana akanipa ono, kasema, "Atapona."

⁹⁷ Ndipo akakutana nami kule, kesho yake asubuhi, Bw. Andrews, naye akanikemea sana. Kasema, "Tumaini la uongo namna hiyo, juu ya mwanamke huyo!"

⁹⁸ Nikasema, "Bw. Andrews, si tumaini la uongo. Mwanamke huyo ni Mkristo. Naye atakapoweza, atakuja kubatizwa."

⁹⁹ Ndipo akasema, "Yuafa." Kasema, "Mimi...Angewezaje kupelekwa nyumbani kutoka Silvercrest?"

¹⁰⁰ Nikasema, "Bwana, unaangalia, unaninii...Kile unachoangalia, unaangalia yale daktari anayosema. Ninaangalia yale Mungu alisema." Unaona?

¹⁰¹ Sasa, hiyo tu ndiyo tofauti, kile unachoangalia. Unaona? Ukiangalia anayosema daktari, hakika utakufa. Bali inakupasa kuangalia yale Mungu aliyosema. Utachukua neno la nani?

¹⁰² Vipi kama Ibrahimu angalichukua maoni ya daktari kuhusu umri wake wa miaka mia moja, na kwamba atampata mtoto kwa mkewe, tisini? Angalifanya nini basi? Mnaona? Mbona, huyo daktari angalisema, "Mtu huyo ana kichaa." Lakini Mungu alimhesabia kwamba ana haki, kwa sababu alimwamini Mungu. Mnaona? Sasa, wewe...

¹⁰³ Ndipo huyo mwanamke akaishi. Alipuuza kubatizwa, Jina la Yesu Kristo, kwa sababu nafikiri kwa namna fulani alikuwa ni Mmethodisti ama Mpresbiteri. Akaanza kuwa mgonjwa zaidi na zaidi. Ndipo akaja akampata Grace Weber, aliyeishi moja kwa moja...ama angali anaishi kule, bintiye anaishi kule. Robe, ndipo akaja hapa, naye akabatizwa katika Jina la Yesu Kristo, akiwa na homa, huku magonjwa ya vivimbe yametokeza kote begani mwake na kila kitu, akiwa na homa, mia moja na nne. Naye akabatizwa papa hapa, katika Jina la Yesu Kristo. Naye anaishi tu ng'ambo ya barabara kutoka hapa. Huenda ameketi hapa sasa. Niliangalia kote nione kama ningeweza kumwona, dakika chache zilizopita. Mnaona? Utii, mnaona.

¹⁰⁴ Sio tu kuzunguka...Ninatofautiana na baadhi ya ndugu zetu, wakiweka tu mikono juu ya *huyu*, *yule*, na *mwingineo*, namna hiyo, na kusema namna fulani ya imani ya ajabu-ajabu itatekeleza hilo. Hilo silo. Inakupasa kuwa na imani halisi, imara ya Roho Mtakatifu, ya Biblia. Unaona? La sivyo, haitadumu. Haidumu.

¹⁰⁵ Hiyo ndiyo sababu ninaweza kumshukuru Bwana kwamba Yeye amenisaidia umbali huu. U—u—uponyaji ambao umefanyika umekuwa ni halisi, kwa sababu wamejengwa kihalisi juu ya BWANA ASEMA HIVI. Mnaona? Kwa hiyo watasimama.

¹⁰⁶ Sasa—sasa, kama maskini shule ya Jumapili...nilikuwa nikingojea kwa dakika moja tu, nikizungumza nanyi, mpaka wakapata mahali pao, kimahali, ili tuweze kutulia sasa. Tuna dakika chache tu, tutaomba, tutaanza kuomba.

¹⁰⁷ Sasa, ninataka kila mmoja wenu ukiri makosa yako kwa Mungu, na kumwahidi Mungu kwamba utamtumikia na kufanya kila uwezacho. Nami pamoja na mchungaji tutaomba, na kuja kuwawekea mikono, nanyi mna hakika ya kuponywa mkiamini.

¹⁰⁸ Watu wale waliokuwa kwenye mikongojo, na viziwi, na bubu, na vipofu, alasiri ya Jumapili iliyopita, wangewezaje kutembea tu hadi jukwaani, wakatupa mikongojo yao; wakatembea hadi jukwaani, macho yakafunguka, mwajua, namna hiyo? Mamia mara mamia yao! Mpaka, nilikuwa dhaifu sana, karibu wanibeba kutoka mahali pale, nikisimama tu, wao wakipitia hapo. Mnaona? Mstari ambao ungetoka hapa mpaka kwenye Shule ya Sekondari ya Juu ya Jeffersonville, karibu hivyo, wamepanga foleni, wakipitia mstarini. Na sijui kama kuna mmoja wao, aliyepitia pale, ila aliyeponywa. Mnaona? Kwa sababu walikuja juu ya msingi wa imani halisi, ya kweli, ya Kikristo na wakiamini. Wao... Halina budi kutendeka.

Sasa inamisheni vichwa vyenu, kila mmoja, mkanisaidie kuwaombea.

¹⁰⁹ Bwana Yesu, tunakuletea Wewe, asubuhi ya leo, kusanyiko hili linalosimama hapa, likingojea, la watoto wagonjwa, wanaoteseke, wenye maumivu makali. Hawana tumaini lolote, wengi wao, Bwana, la kuponywa na daktari, hasa sana mtu huyu aliyelala hapa kwenye kitanda hiki cha wagonjwa. Ama ni neema Yako au atoke humu ulimwenguni katika siku chache. Na hapana shaka, huenda kukawa na wengine wamesimama hapa madhabahuni, huku mishtuko ya moyo ikiwangojea, na magonjwa, na mateso ambayo yanguwararua vipande-vipande.

¹¹⁰ Kuna jambo moja tu, Baba, linaloweza kuwaokoa, hilo ni, waende zaidi ya hizi hisi tano hapa za mwili huu, ambapo madaktari wamejaribu kwa uaminifu, hapana shaka, kuyaokoa maisha yao; magonjwa, kansa, TB, ugonjwa wa moyo. Na pamoja na viraka vyote, na matyubu, na vifaa, na—na—na dawa za kupigana na viini, adui hujilundika moja kwa moja mle ndani, apate kuyachukua maisha yao.

¹¹¹ Nami nimeelezea, Bwana, ninaamini, maoni Yako, kwao. Nami nimemsikia mtu huyu akinena kwa lugha asubuhi ya leo, na kutoa tafsiri hiyo, kile kingetukia leo hii. Baadhi yao wataupokea, Bwana, hakika. Hiyo ni kweli. Ninaamini.

¹¹² Na sasa, kama ilivyoandikwa katika Biblia, ya kwamba Daudi, yule maskini mvulana mchungaji, alikuwa akiwachunga kondoo wa baba yake, huko nje nyuma ya jangwa. Ndipo siku moja simba akaingia na kumchukua mmoja wa wana-kondoo wa baba yake, na kukimbia naye. Naye huyo mvulana

mdogo mchungaji, pamoja na imani, yeye alikuwa na nini kumkabili simba huyu? Si silaha ya siku hizi wala bunduki. Bali alikuwa na kombeo dogo, ndipo akamfuatilia huyo simba. Akamwua huyo simba, na kumrudisha huyo kondoo. Dubu aliingia akamshika mmoja; akamfuatilia dubu huyo ambaye angaliweza kumvunjilia ardhini. Lakini yeye hakuwazia juu ya ukubwa wa huyo dubu, wala nguvu za huyo simba, wala mbio zake, wala kutoweza kwake kutumia hilo kombeo.

¹¹³ Lakini wakati alipokuwa amesimama mbele za mfalme Sauli, yeye alisema, “Mtumishi wako aliwachunga kondoo wa baba yake, naye simba akaingia na kuchukua mmoja, na kukimbia. Nami nikamfuatilia na kumrudisha huyo kondoo.” Akasema, “Mungu yeye yule aliyeniokoa mkononi, ama kwenye wayo wa huyo dubu, ama meno ya huyo simba, anaweza pia kumchukua Mfilisti huyu asiyetahiriwa na kumkabidhi mkononi mwangu.”

¹¹⁴ Jinsi tunavyojua hiyo hadithi inavyoenenda, kwamba kweli alimwua; akamwua mtu aliyekuwa mkubwa mara nyingi, nyingi sana kuliko yeye alivyokuwa, na ni shujaa. Jinsi lilivyomtatiza Sauli, mfalme yule mkuu, mtu mashuhuri, mwenye nguvu, jinsi ambavyo mvulana huyo mdogo angeweza kuwa na imani kama hiyo katika kombeo. La, si katika kombeo, bali katika Mungu.

¹¹⁵ Sasa, Bwana, wakisimama kwenye madhabahu haya, wakiketi kwenye kitanda hiki cha wagonjwa, ni kondoo wa Mungu, wana-kondoo wadogo, tuseme, Kwake. Wameshikwa na simba anayeitwa kansa, dubu anayeitwa TB, magonjwa mengine ambayo yamewashika, na kuwanyakua, na kuwararua vipande-vipande. Bwana, ni—ninawafuatilia, kwa kombeo dogo linaloitwa maombi ya imani. Si makubwa sana, bali ninajua kile yamefanya. Nami ninajua angali ni Mungu yeye yule. Ninawafuatilia, asubuhi ya leo, nipate kuwarejesha, Bwana, kwenye malisho ya majani mabichi ya afya njema, huko chini karibu na maji matulivu ya amani, na mbali na mahangaiko yao, wapate kukuamini Wewe.

¹¹⁶ Nami ninawafuatilia, kwa silaha ambayo Wewe ulitoa ya kuingia nayo. “Kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, naye Mungu atawainua. Kama wametenda dhambi yoyote, watasamehewa.”

¹¹⁷ Na, Baba, tunaenda sasa kukabiliana na adui, kukabiliana na simba, kukabiliana na i—ibilisi katika kila hali aliyomo, anayeitwa kansa, TB, ugonjwa wa Hodgkin, ugonjwa wa moyo, ugonjwa mwingine wowote. Tunakuja kumtafuta, na kumrejesha mwana-kondoo huyu Nyumbani mwa Mungu tena. Katika Jina la Yesu Kristo tunaenda, kulitumia kombeo hili ambalo ulitupa Wewe. Kuwa pamoja nasi, Baba, tunapokukaribia Wewe kwa uchaji sasa, katika Jina la Yesu.

¹¹⁸ Ninawataka mwendeleee kuinamisha vichwa vyenu. Nasi tunakuja kutia mafuta, na kuwawekea mikono wagonjwa, na maombi ya imani yatamwokoaa mgonjwa huyo. Kila Mkristo aliye humu ndani, weka imani yako katika mstari huu wa maombi.

¹¹⁹ [Ndugu Branham anaondoka kwenye maikrofoni ya mimbarani kwa dakika tatu na nusu, wakati yeye na Ndugu Neville wakiwaombea wagonjwa, ila maneno fulani ya maombi ya Ndugu Branham hayawezi kusikika, aya 119-122. Mcheza piano anaendelea kucheza *Amini Tu* mpaka maombi yamekwisha—Mh.]

Katika Jina la Yesu Kristo!

Katika Jina la Yesu Kristo!

Jina la Yesu!

Jina la Yesu Kristo!

Jina la Yesu!

Baba, namkemea ibilisi! . . . ? . . .

Katika Jina la Yesu Kristo!

Katika Jina la Yesu Kristo! . . . ? . . .

Katika Jina la Yesu Kristo!

Njoo na uliamini . . . ? . . . na litatendeka! . . . ? . . .

Bwana, Wewe . . . ? . . .

Mungu . . . ? . . .

¹²⁰ Bwana, Wewe ni . . . Uliandika ile nafasi. Wewe ni wa Jamaa, Kristo! . . . ? . . . Katika Jina la Yesu Kristo!

¹²¹ “Maombi ya imani yatamwokoaa mgonjwa yule.” Ninataka Wewe umfanyie. Umrudishe awe mwanamke mwenye afya! . . . ? . . .

Jina la Yesu Kristo, mrudishe!

Katika Jina la Yesu Kristo, mrudishe! . . . ? . . .

Katika Jina la Yesu Kristo, kumrudisha dada yangu.

Katika Jina la Yesu Kristo, kumrudisha ndugu yangu! . . . ? . . .

Katika Jina la Yesu Kristo! . . . ? . . .

Katika Jina la Yesu Kristo! . . . ? . . .

Katika Jina la Yesu Kristo! . . . ? . . .

Kamwe hukufanya. Bwana akubariki!

Ninamfuatilia, asubuhi ya leo! . . . ? . . .

¹²² Katika Jina la Yesu Kristo, ninakurudisha, kwa maombi ya imani, kutoka utumwani! . . . ? . . . Tunaongezea imani yetu kwa hawa! . . . ? . . .

[Ndugu Branham anarudi kwenye maikrofoni ya mimbarani—Mh.]

Amini tu;

Huku vichwa vyetu vimeinamishwa sasa, sasa.

Amini tu, amini tu,

Mambo yanawezekana, amini tu.

Ee Bwana, naamini; Ee Bwana, naamini;

Mambo yote yawezekana . . .

Na tuinue tu mikono yetu sasa.

. . . Bwana, naamini;

Ee Bwana, naamini; Bwana, naamini;

Mambo yote yawezekana, Bwana, naamini.

¹²³ Baba yetu wa Mbinguni, wale walioweza kusimama, waliinua mikono yao, kwamba walikuwa wamelikubali. Ndugu huyu aliyekuwa amelala kwenye kitanda cha wagonjwa, aliamka, kuonyesha ya kwamba alikuwa ameukubali uponyaji wake. Tunaamini, Bwana, wanatembea wakirudi kwa amani sasa kwenye kivuli cha malisho ya majani mabichi, kando ya maji matulivu, wapate kuwa wazima tena, kwa Jina la Yesu. Tunakushukuru Wewe kwa ajili yake. Amina.

¹²⁴ Vema, Ndugu Neville, nitaketi hapa na kukusikiliza ukihubiri sasa.



NG'AMBO YA PAZIA LA WAKATI SWA61-0305

(Beyond The Curtain Of Time)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 5 Machi, 1961, kwenye Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyoerekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org